



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Ushirikiano baina ya UNESCO, MUHAS na Wizara ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto katika kukuza Utabibu Mtandao kuendeleza uvumbuzi katika Sekta ya Afya Tanzania

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi-Muhimbili, UNESCO pamoja na wadau wengine muhimu watakutana, tarehe 16 Mei 2017, Kampasi ya Muhimbili (MUHAS), ili kubuni dhana mpya kwa ajili ya utoaji huduma za afya kwa njia ya mtandao katika kijiji cha Wamasai, Mkoani Arusha.

Huu ushirikiano utaendeleza utoaji wa huduma bora za afya, zenye ufanisi wa kitaalamu zaidi katika maeneo ya vijijini, ambayo mara nyingi huachwa nyuma katika utoaji wa huduma hizo. Dhana ya utabibu mtandao inalenga hasa kuiinua utumiaji wa teknolojia ya kidigitali ya kisasa, ambapo utekelezaji wake utakuwa mfano elekezi wa kuboresha matumizi ya teknolojia katika karne ya ishirini na moja katika maendeleo ya utoaji wa huduma za afya nchini na barani Afrika.

Majaribio haya yanafuata juhudi za UNESCO zilizoanzishwa kwa msaada wa Samsung na mamlaka za wilaya ya Ngorongoro. Juhudi hizo zilipelekea kuanzishwa kwa Kliniki ya Diigitali, kama jukwaa halisia la uvumbuzi mpya la kupima viwango na utoaji wa huduma za afya ya mama na mtoto na afya ya kinywa, masikio, pua na koo (ENT) zinazotumia teknolojia ya kisasa. Kliniki ya Digitali ilizinduliwa katika kijiji cha Ololosokwan Ngorororo, Arusha mnamo mwezi Novemba mwaka 2016.

Warsha ijayo itatoa mwelekeo wa awamu ya pili ya mpango huu kwa kuwakutanisha wabunifu, wataalamu wa afya na wanateknolojia ili kudadavua dhana ya utekelezaji kamilifu wa jaribio ya utoaji wa huduma za afya kwa kutumia teknolojia ya kisasa, na baadaye kuirasimisha kama mfumo ya kuboresha afya katika maeneo zilizoko pembezoni ya miji na vijijini. Jaribio la utoaji wa huduma za afya kwa njia ya mtandao litakuwa ni la kwanza litakalounganisha ngazi mbalimbali za mfumo wa huduma za afya Tanzania. Itakua pia, mfano wa mfumo bora wa kuunganisha huduma za afya kwa kanda zote za Tanzania. Mbinu na zana mpya zitakazounganisha zahanati vijijini na mifumo ya kitaifa na kimataifa ya huduma za afya na mafunzo zitalenga upanuzi wa wigo wa kuwafikia wakazi wa vijijini na huduma za kitaaluma zaidi za afya. Juhudi maalum pia zitalenga utolewaji wa msaada kwa ajili ya maendeleo ya sehemu ya upanuzi wa wigo wa matibabu maalum yanayohitaji taaluma.

Sambamba na hilo, MUHAS na UNESCO watasaini Mkataba wa Makubaliano ya kurasimisha ushirikiano wao katika uendeshwaji wa mradi mzima wa Kijiji cha Uvumbuzi wa Dijitali ya Afya. Makubaliano haya yataadhimisha pia hatua muhimu katika utekelezaji wa Uwenyekiti wa maswala ya Utabibu Mtandao uliyotolewa hivi karibuni na UNESCO kwa Chuo cha Muhimbili.

Wageni rasmi watakaohudhuria mkutano huo ni pamoja na Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk Mpoki Ulisubisya, Makamu Mkuu wa Chuo cha Muhimbili, Profesa Ephata Kaaya na Mwakilishi Mkazi wa UNESCO, Bi Zulmira Rodrigues. Wataungana na wakuu wa taasisi mbalimbali wengine kama Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Naibu Katibu Mkuu wa Afya, Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, watu binafsi wanaowakilisha mashirika kama vile The Africa Foundation, Aga Khan Foundation, Ubalozi wa Uswisi na Bill & Melinda Gates Foundation, pamoja na Maafisa wa Afya wa mkoa na wilaya za Arusha na Ngorongoro watashiriki.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

UNESCO Dar Office, Tanzania | Tiina Neuvonen | +255 7 433 016 80| te.neuvonen@unesco.org

MUHAS | Felix Sukums | +255 7 13238473 | sukums@gmail.com

MHCDCGEV, Dr. Liggy Vumilia | +255 767 467 455 | liggyv@yahoo.com